

HABARI NJEMA



Gode Nyheder




Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu. Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe. Naye akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwana-mume; na jina lake utamwita Yesu. Huyu atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho. Mariamu akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema. Kisha malaika akaondoka akaenda zake.

(Luka Mtakatifu 1:26-33 & 38)

I den sjette måned derefter blev engelen Gabriel sendt fra Gud til en by i Galilæa, som hedder Nazaret, til en jomfru, som var trolovet med en mand ved navn Josef, af Davids hus; og jomfruens navn var Maria. Og engelen kom ind til hende og sagde: »Vær hilset, du benådede, Herren er med dig! du velsignede blandt kvinder.« Men hun blev forfærdet over de ord og tænkte ved sig selv, hvad denne hilsen skulle betyde. Da sagde engelen til hende: »Frygt ikke, Maria! thi du har fundet nåde for Gud, og se, du skal undfange og føde en søn, og du skal give ham navnet Jesus. Han skal blive stor og kaldes den Højstes Søn; og Gud Herren skal give ham Davids, hans faders, trone. Han skal være konge over Jakobs hus til evig tid, og der skal ikke være ende på hans kongedømme.« Da sagde Maria: »Se, jeg er Herrens tjenerinde; mig ske efter dit ord!« Så forlod engelen hende.

(Lukas 1:26-33 & 38)




Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi mpaka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi; ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amem-
posa, naye ana mimba. Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, akanzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.

(Luka Mtakatifu 2:4-7)

Og fordi Josef var af Davids hus og slægt, drog også han op fra Galilæa, fra byen Nazaret, til Judæa, til Davids by, som hedder Betlehem, for at lade sig indskrive tillige med Maria, sin trolovede, som var frugtsommelig. Og det skete, medens de var der, kom tiden, da hun skulle føde. Og hun fødte sin Søn, den førstefødte, og svøbte ham og lagde ham i en krybbe, thi der var ikke plads til dem i herberget.

(Lukas 2:4-7)



Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondenini na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe. Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia. (Luka Mtakatifu 2:8-14)

I den samme egn var der hyrder, som lå ude på marken og holdt nattevagt over deres hjord. Og en Herrens engel stod for dem, og Herrens herlighed strålede om dem, og de blev grebet af stor frygt. Men engelen sagde til dem: »Frygt ikke; thi se, jeg forkynder eder en stor glæde, som skal være for hele folket. Thi eder er i dag en frelser født i Davids by; han er Kristus, Herren! Og dette skal være jer et tegn: I skal finde et barn svøbt og liggende i en krybbe.« Og i det samme var der med engelen en mangfoldig himmelsk hærskaar, som lovpriste Gud og sagde: »Ære være Gud i det højeste! og på jorden fred i mennesker, der har hans velbehag!« (Lukas 2:8-14)



Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na
neema ya Mungu ilikuwa juu yake. (Luka Mtakatifu 2:40)

Og barnet voksede og blev stærkt og fyldtes af visdom; og Guds
nåde var over det. (Lukas 2:40)



Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi. Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao. Na Yohana alikuwa amevaa singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake, akala nzige na asali ya mwitu. Akahubiri akisema, Yuaja nyuma yangu aliye na nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuinama na kuilegeza gidamu ya viatu vyake. Mimi niliwabatiza kwa maji; bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu. Ikawa siku zile, Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani. Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka, na Roho, kama hua, akishuka juu yake; na sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe. (Marko Mtakatifu 1:4-11)

Således fremstod Johannes Døber i ørkenen og prædikede omvendelsesdåb til syndernes forladelse. Og hele Judæas land og alle Jerusalems indbyggere kom dragende ud til ham, og de lod sig døbe af ham i Jordanfloden, idet de bekendte deres synder. Johannes var iført en kamelhårs klædning og havde et læderbælte om livet, og han levede af græshopper og vilde biers honning. Og han prædikede og sagde: »Efter mig kommer han, som er stærkere end jeg; jeg er end ikke værdig til at bøje mig ned og løse remmen på hans sko. Jeg har døbt jer med vand, men han skal døbe jer med Helligånd.« Og det skete i de dage, at Jesus kom fra Nazaret i Galilæa. Og han blev døbt af Johannes i Jordan. Og straks, da han steg op af vandet, så han himlene skilles ad, og han så Ånden dale ned over sig som en due. Og der lød en røst fra Himlene: »Du er min Søn, den elskede, i dig har jeg velbehag.« (Markus 1:4-11)



Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, tena wawe na amri ya kutoa pepo.
(Marko Mtakatifu 3:13-15)

Og han går op i bjergene og kalder dem til sig, han selv ønskede at have med, og de kom til ham. Og han indsatte tolv til at være hos ham, og for at han kunne udsende dem til at prædike med magt til at uddrive de onde ånder.
(Markus 3:13-15)




Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi. Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye. Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.

(Yohana Mtakatifu 3:1-6)

Der var blandt farisæerne en mand, som hed Nikodemus, en af jødernes rådsherrer. Han kom til Jesus om natten og sagde til ham: »Rabbi! vi ved, at du er en lærer, som er kommen fra Gud; thi ingen kan gøre de tegn, som du gør, uden Gud er med ham.« Jesus svarede og sagde til ham: »Sandelig, sandelig siger jeg dig: ingen kan se Guds rige, hvis han ikke bliver født på ny.« Nikodemus siger til ham: »Hvorledes kan et menneske fødes, når det er gammelt? Det kan da ikke for anden gang komme ind i sin moders liv og fødes?« Jesus svarede: »Sandelig, sandelig siger jeg dig: ingen kan komme ind i Guds rige, hvis han ikke bliver født af vand og Ånd. Hvad der er født af kødet, er kød; og hvad der er født af Ånden, er Ånd.«

(Johannes 3:1-6)



Baadaye kidogo alikwenda mpaka mji mmoja uitwao Naini, na wanafunzi wake walifuatana naye pamoja na mkutano mkubwa. Na alipolikaribia lango la mji, hapo palikuwa na maiti anachukuliwa nje, ni mwana pekee wa mamaye ambaye ni mjane, na watu wa mjini wengi walikuwa pamoja naye. Bwana alipomwona alimwonea huruma, akamwambia, Usilie. Akakaribia, akaligusa jeneza; wale waliokuwa wakilichukua wakasimama. Akasema, Kijana, nakuambia, Inuka. Yule maiti akainuka, akaketi, akaanza kusema. Akampa mama yake.

Hofu ikawashika wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Nabii mkuu ametokea kwetu; na, Mungu amewaangalia watu wake. (Luka Mtakatifu 7:11-16)

Det skete engang i tiden derefter, at han gik til en by, som hed Nain, og hans disciple og en stor skare ledsagede ham. Men da han nærmedesig byens port, se, da blev en død båret ud, en moders eneste søn, og hun var enke. Ogen hel skare fra byen fulgte med hende. Da Herren så hende, ynkedes han inderligt over hende og sagde til hende: »Græd ikke!« Og han gik hen og rørte ved båren; og de, som bar den, standsede. Da sagde han: »Unge mand, jeg siger dig: stå op!« Og den døde satte sig op og begyndte at tale; og han gav ham til hans moder. Da blev alle grebet af frygt, og de priste Gud og sagde: »En stor profet er fremstået iblandt os, og Gud har besøgt sit folk.« (Lukas 7:11-16)



Basi Yesu alipoinua macho yake akaona mkutano mkuu wanakuja kwake, alimwambia Filipo, Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula? Na hilo alilina ili kumjaribu; kwa maana alijua mwenyewe atakalotenda. Filipo akamjibu, Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi, kila mmoja apate kidogo tu. Wanafunzi wake mmojawapo, Andrea, nduguye Simoni Petro, akamwambia, Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa? Yesu akasema, Waketisheni watu. Na mahali pale palikuwa na majani tele. Basi watu waume wakaketi, wapata elfu tano jumla yao. Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka. Nao waliposhiba, aliwambia wanafunzi wake, Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee cho chote. Basi wakavikusanya, wakajaza vikapu kumi na viwili, vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyowabakia wale waliokula. Basi watu wale, walipoiona ishara aliyoifanya, walisema, Hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimwenguni. (Yohana Mtakatifu 6:5-14)

Da Jesus nu så op og fik øje på en stor folkeskare, som kom hen imod ham, siger han til Filip: »Hvor skal vi købe brød, så alle disse kan få noget at spise?« Men dette sagde han for at sætte ham på prøve; thi selv vidste han, hvad han ville gøre. Filip svarede ham: »For to hundrede denarer brød er ikke nok til dem, så de hver kan få blot en smule.« En anden af hans disciple, Andreas, Simon Peters broder, siger til ham: »Her er en lille dreng, som har fem bygbrød og to fisk; men hvad er det til så mange?« Jesus sagde: »Lad folkene sætte sig ned.« Og der var meget græs dér på stedet. Da satte mændene sig ned, omtrent fem tusinde i tallet. Jesus tog nu brødene, takkede og delte dem ud til dem, som havde sat sig; ligeledes også af fiskene så meget, som de ville have. Og da de var blevet mætte, siger han til sine disciple: »Saml de tiloversblevne stykker sammen, så intet går til spilde.« Så samlede de sammen og fyldte tolv kurve med de stykker, som de, der havde fået mad, havde levnet af de fem bygbrød. Da nu folkene så det tegn, han havde gjort, sagde de: »Han er i sandhed den profet, der kommer til verden.« (Johannes 6:5-14)



Hata ilipokuwa jioni wanafunzi wake wakatelemka baharini; wakapanda chomboni, wakaanza kuivuka bahari kwenda Kapernaumu. Nako kumekwisha kuwa giza, wala Yesu hajawafikia. Na bahari ikaanza kuchafuka kwa kuvuma upepo mkuu. Basi wakavuta makasia kadiri ya maili tatu nne, wakamwona Yesu anakwenda juu ya bahari na kukikaribia chombo; wakaogopa. Naye akawaambia, Ni mimi, msiogope. Basi wakataka kumpokea chomboni; na mara hiyo chombo kikaifikilia nchi waliyokuwa wakiiendea. (Yohana Mtakatifu 6:16-20)

Men da det blev aften, gik hans disciple ned til søen. Og de gik om bord i en båd og ville sætte over til Kapernaum på den anden side af søen. Men det var allerede blevet mørkt, og Jesus var endnu ikke kommen til dem. Søen gik højt, da der blæste en stærk vind. Da de nu havde roet femogtyve til tredive stadier, får de øje på Jesus, der vandrer på søen og nærmer sig båden, og de blev grebet af frygt. Men han siger til dem: »Det er mig; frygt ikke!« Så ville de tage ham op i båden; og straks landede båden ved den bred, de var sejlet over til. (Johannes 6:16-21)



Basi wakamletea watoto wadogo ili awaguse; wanafunzi wake wakawakemea. Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa. Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia. (Marko Mtakatifu 10:13-16)


De bar nogle små børn til ham, for at han skulle røre ved dem; men disciplene truede ad dem. Men da Jesus så det, harmedes han og sagde til dem: »Lad de små børn komme til mig; dem må I ikke hindre; thi Guds rige hører sådanne til. Sandelig siger jeg eder: den, der ikke tager imod Guds rige ligesom et lille barn, han kommer slet ikke ind i det.« Og han tog dem i favn og lagde hænderne på dem og velsignede dem. (Markus 10:13-16)



Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wani-fuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. (Yohana Mtakatifu 10:11 & 27-28)

»Jeg er den gode hyrde; den gode hyrde sætter sit liv til for fårene. Mine får hører min røst, og jeg kender dem, og de følger mig. Og jeg giver dem evigt liv, og de skal i al evighed ikke fortabes, og ingen skal rive dem ud af min hånd.«

(Johannes 10:11 & 27-28)



Basi wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakakusanya baraza, wakasema, Tunafanya nini? Maana mtu huyu afanya ishara nyingi. Tukimwacha hivi, watu wote watamwamini; na Warumi watakuja, watatuondolea mahali petu na taifa letu. Mtu mmoja miongoni mwao, Kayafa, aliyekuwa Kuhani Mkuu mwaka ule, akawaambia, Ninyi hamjui neno lo lote; wala hamfikiri ya kwamba yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima. Na neno hilo yeye hakulisema kwa nafsi yake; bali kwa kuwa alikuwa Kuhani Mkuu mwaka ule, alitabiri ya kwamba Yesu atakufa kwa ajili ya taifa hilo. Wala si kwa ajili ya taifa hilo tu; lakini pamoja na hayo awakusanye watoto wa Mungu waliotawanyika, ili wawe wamoja. Basi tangu siku ile walifanya shauri la kumwua. (Yohana Mtakatifu 11:47-53)


Ypperstepræsterne og farisæerne kaldte da rådet sammen og sagde: »Hvad skal vi gøre? Den mand gør jo mange tegn. Hvis vi lader ham blive sådan ved, vil alle tro på ham, og romerne vil komme og tage både land og folk fra os.« Men en af dem, Kajfas, som var ypperstepræst det år, sagde til dem: »I forstår da heller ingenting! og I tænker heller ikke på, at det er bedre for jer, at ét menneske dør for folket, end at hele folket går til grunde!« Dette sagde han ikke af sig selv; men da han var ypperstepræst i det år, profeterede han, at Jesus skulle dø for folket; og ikke for folket alene, men også for at samle Guds adspredte børn sammen til ét. Fra den dag af var deres beslutning taget, at de ville slå ham ihjel.

(Johannes 11:47-53)




Basi kulipokuwa jioni aliketi chakulani pamoja na wale Thenashara. Nao walipokuwa wakila, alisema, Amin, nawaambia, Mmoja wenu atanisaliti. Wakahuzunika sana, wakaanza kumwuliza mmoja mmoja, Ni mimi, Bwana? Akajibu akasema, Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakayenisaliti. (Mathayo Mtakatifu 26:20-23)

Da det no var blevet aften, satte han sig til bords med de tolv. Og mens de spiste, sagde han: »Sandelig siger jeg eder: en af jer vil forråde mig.« Da blev de meget bedrøvede og begyndte hver især at spørge ham: »Det er dog vel ikke mig, Herre?« Han svarede og sagde: »Han, som nu sammen med mig stak hånden i fadet, han vil forråde mig.« (Mattæus 26:20-23)






Wakapelekwa na wawili wengine, wahalifu, wauawe pamoja naye. Na walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulibisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume, na mmoja upande wa kushoto. Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana, akisema, Je! wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu, akamkemea, akisema, Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa. Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia, Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.
(Luka Mtakatifu 23:32-33 & 39-43)

Desuden blev også to forbrydere ført ud for at henrettes sammen med ham. Og da de var kommet til det sted, som kaldes »Hovedskal«, korsfæstede de ham dér tillige med forbryderne, den ene ved hans højre, den anden ved hans venstre side. Og en af forbryderne, som hang der, spottede ham: »Er du ikke Kristus? Frels dig selv og os!« Da tog den anden til orde og irettesatte ham og sagde: »Frygter end ikke du Gud, skønt du er under den samme dom? Og vi er det med rette; vi får jo kun løn som forskyldt; men denne mand har intet ondt gjort.« Og han sagde: »Jesus! kom mig i hu, når du kommer i dit rige!« Da svarede han ham: »Sandelig siger jeg dig: i dag skal du være med mig i Paradis.«
(Lukas 23:32-33 & 39-43)




Hapo ilikuwa yapata saa sita, kukawa giza juu ya nchi yote hata saa kenda, jua limepungua nuru yake; pazia la hekalu likapasuka katikati. Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema, Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu. Alipokwisha kusema hayo alikata roho. Yule akida alipoona yaliyotukia, alimtukuza Mungu, akisema, Hakika yake, mtu huyu alikuwa mwenye haki. (Luka Mtakatifu 23:44-47)

Det var nu ved den sjette time, og der blev mørke over hele landet indtil den niende time, idet solen formørkedes. Og forhængene i templet flængedes midt igennem. Og Jesus råbte med høj røst og sagde: »Fader! i dine hænder betror jeg min ånd;« og da han havde sagt det, udåndede han. Men da høvedsmanden så, hvad der skete, priste han Gud og sagde: »Det var i virkeligheden en retfærdig mand.«
(Lukas 23:44-47)



Hata ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu, naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu; mtu huyu alimwendea Pilato, akauomba mwili wa Yesu. Ndipo Pilato akaamuru apewe. Yusufu akautwaa mwili, akauzongazonga katika sanda ya kitani safi, akauweka katika kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani; akavingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake. Na pale walikuwapo Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, wameketi kulielekea kaburi. (Mathayo Mtakatifu 27:57-61)

Men da det var blevet aften, kom der en rig mand fra Arimatæa, ved navn Josef, som selv var blevet discipel af Jesus. Han gik til Pilatus og bad om at få Jesu legeme. Da befalede Pilatus, at det skulle udleveres. Og Josef tog hans legeme og svøbte det i et rent liglagen og lagde det i den nye grav, som han havde ladet hugge ud i klippen til sig selv. Så væltede han en stor sten for indgangen til graven og gik bort. Maria Magdalene og den anden Maria var til stede og sad lige over for graven. (Mattæus 27:57-61)





Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari. Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi, wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu. Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajili ya neno hilo, tazama, watu wawili walisimama karibu nao, wamevaa nguo za kumetameta; nao walipoiingiwa na hofu na kuinama kifudifudi hata nchi, hao waliwaambia, Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya, akisema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu. Wakayakumbuka maneno yake.

(Luka Mtakatifu 24:1-8)


Men ved daggry på den første dag i ugen kom de til graven med de vellugtende salver, som de havde tilberedt. Og de fandt stenen væltet bort fra graven. Men da de gik derind, fandt de ikke Herren Jesu legeme. Og da de stod rådvilde over for dette, se, da skete det, at der stod to mænd hos dem i strålende klædebon. Da de blev forfærdede og bøjede deres ansigter mod jorden, sagde mændene til dem: »Hvorfor leder I efter den levende blandt de døde? Han er ikke her, men han er opstanden; kom i hu, hvorledes han talte til jer, da han endnu var i Galilæa, og sagde, at Menneskesønnen skulle overgives i syndige menneskers hænder og korsfæstes og opstå på den tredje dag.«

(Lukas 24:1-8)



Wakaondoka saa ile ile, wakarejea Yerusalemu, wakawakuta wale kumi na mmoja wamekutanika, wao na wale waliokuwa pamoja nao, wakisema, Bwana amefufuka kweli kweli, naye amemtokea Simoni. Nao waliwapa habari ya mambo yale ya njiani, na jinsi alivyotambulikana nao katika kuumega mkate. Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu. Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, Mbona mnafadhaika? na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake. (Luka Mtakatifu 24:33-40)

Så brød de op i samme stund og vendte tilbage til Jerusalem og fandt dér de elleve og deres fæller forsamlede, som sagde: »Herren er virkelig opstanden og set af Simon.« Og selv fortalte de, hvad der var sket på vejen, og hvordan de havde genkendt ham, da han brød brødet. Medens de talte om dette, stod han selv midt iblandt dem og siger til dem: »Fred være med eder!« Da blev de grebet af angst og frygt og mente, det var en ånd, de så. Men han sagde til dem: »Hvorfor er I forfærdede? og hvorfor opstiger der tvivl i jeres hjerter? Se på mine hænder og mine fødder, at det er mig selv; føl på mig og se; en ånd har jo ikke kød og ben, som I ser, jeg har.« [Og da han havde sagt dette, viste han dem sine hænder og sine fødder.] (Lukas 24:33-40)



Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Akawaongoza mpaka Bethania, akainua mikono yake akawabariki. Ikawa katika kuwabariki, alijitenga nao; akachukuliwa juu mbinguni. (Luka Mtakatifu 24:46-48 & 50-51)

Og han sagde til dem: »Således står der skrevet, at Kristus skal lide og opstå fra de døde på den tredje dag, og at der i hans navn skal prædikes omvendelse til syndernes forladelse for alle folkeslagene og begyndes fra Jerusalem. I skal være vidner om dette.« Så tog han dem med sig ud, hen i nærheden af Betania, og han løftede sine hænder og velsignede dem. Og det skete, medens han velsignede dem, skiltes han fra dem og opløftedes til Himmelen. (Lukas 24:46-48 & 50-51)

Thi således elskede Gud verden, at han gav sin Søn den enbårne, for at enhver, som tror på ham, ikke skal fortabes, men have evigt liv. Thi Gud sendte ikke sin Søn til verden for at dømme verden, men for at verden skal frelses ved ham. Den, som tror på ham, dømmes ikke; den, som ikke tror, er allerede dømt, fordi han ikke har troet på Guds enbårne Søns navn. (Johannes 3:16-18)

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. (Yohana Mtakatifu 3:16-18)

Hvis vi bekender vore synder, er han trofast og retfærdig, så han tilgiver os vore synder og renses os fra al uretfærdighed. Hvis vi siger, at vi ikke har syndet, så gør vi ham til en løgner, og hans ord er ikke i os. (I Johannes 1:8-9)

Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. (I Yohana 1:8-9)

Jesus svarer: »Jeg er vejen og sandheden og livet; ingen kommer til Faderen uden ved mig.« (Johannes 14:6)

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. (Yohana Mtakatifu 14:6)

»Kom hid til mig, alle I, some er trætte og tyngede af byrder, og jeg vil give jer hvile. Tag mit åg på jer og lær af mig, thi jeg er sagtmodig og ydmyg af hjertet; så skal I finde hvile for jeres sjæle. Thi mit åg er gavnligt, og min byrde er let.« (Mattæus 11:28-30)

Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi. (Mathayo Mtakatifu 11:28-30)

Endnu mange andre tegn, som ikke er nedskrevet i denne bog, gjorde Jesus for øjnene af sine disciple. Men disse er nedskrevet, for at I skal tro, at Jesus er Kristus, Guds Søn, og for at I, når I tror, skal have livet i hans navn. (Johannes 20:30-31)

Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa; ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake. (Yohana Mtakatifu 20:30-31)

»Jeg er Alfa og Omega, den første og den sidste, begyndelsen og enden.« (Johannes' Åbenbaring 22:13)

Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho. (Ufunuo Wa Yohana 22:13)

AΩ



Om følgende bøn, udtrykker dine ønsker og længsler, så kan du bede denne bøn og Jesus vil komme ind i dit liv, som Han har lovet:

"Kære Herre Jesus, jeg forstår at jeg er en synder som trænger til Dig! Jeg takker dig at Du døde på korset for mine synder! Tak at du tilgiver mig mine synder og giver mig evigt liv. Jeg beder Dig derfor, komme ind og råde over hele mitt liv som min Frelser og Herre, Amen"

Navn: _____ Dato: _____

Je maombi haya ni sawa na moyo wako? Kama ni sawa, omba maombi haya na Kristo ataingia ndani ya maisha yako kama alivyoahidi:

"Bwana Yesu, Nimegundua ya kwamba mimi ni nwenye dhambi na ninakuhitaji katika maisha yangu. Ninakushukuru kwa kufa msalabani ili uondoe dhambi zangu. Asante kwa kunisamehe na kunipa maisha ya milele. Ninakukaribisha ndani ya maisha yangu kama Bwana na Mwokozi. Tafadhali yaongoze maisha yangu."

Jina _____ Tarahe _____

Ime Pigwa: Linda Riddell
Illustrated by: Linda Riddell

www.goodnewscoloringbook.org

Swahili/Danish

